# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
# MAHKAMA

**SIMU: 024-2230182**
**FAX: 024-2232720**
**S.L.P: 160**
**e- mail: jsc@judiciaryzanzibar.go.tz**

**OFISI YA TUME YA UTUMISHI WA MAHKAMA**
**214 BARABARA YA TUNGUU**
**70491 KUSINI UNGUJA**
**ZANZIBAR**

**TAREHE 14/07/2026**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Tume ya Utumishi ya Mahkama inatangaza nafasi za kazi kwa Mahkama Zanzibar katika kada zifuatazo:

### 1. HAKIMU WA MKOA (ZPS-EX - 41)

**NAFASI SABA (7) UNGUJA NA NAFASI TATU (3) PEMBA.**

**Sifa za muombaji**

a) Awe amehitimu shahada ya kwanza katika fani ya Sheria kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.
b) Awe na uzoefu usiopungua miaka mitano katika fani ya Sheria
c) Uwezo wa kutumia Kompyuta ni sifa ya ziada itakayopewa kipaumbele.
d) Awe Mzanzibari.

**Majukumu**

i. Kusikiliza kesi za madai, jinai pamoja rufaa kwa mujibu wa uwezo aliopewa kisheria.
ii. Kutoa amri mbali mbali za kimahkama anazoruhusiwa kisheria.
iii. Kuandaa taarifa zinazohusiana na usikilizaji wa mashauri mbali mbali katika Mahkama ya Mkoa.

iv. Kufuatilia na kuandaa majibu ya hoja mbali mbali zinazotokana na malalamiko ya wananchi kuhusiana na huduma za mahkama.

**2. KADHI WA MKOA (ZPS-EX -41)**

**NAFASI TATU (3) UNGUJA NA NAFASI MBILI (2) PEMBA.**

**Sifa za muombaji**

a) Awe amehitimu shahada ya kwanza katika fani ya Sharia ya kiislamu kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

b) Awe na uzoefu usiopungua miaka mitano katika fani ya Sharia

c) Uwezo wa kutumia Kompyuta ni sifa ya ziada itakayopewa kipaumbele.

d) Awe Mzanzibari.

**Majukumu**

i. Kusikiliza kesi za madai zinazohusiana na mambo ya kiislamu kwa mujibu wa uwezo aliopewa kisheria.

ii. Kusikiliza kesi za rufaa zinazotoka Mahkama za Kadhi za Wilaya.

iii. Kusimamia upatikanaji wa mienendo ya kesi pamoja na utekelezaji wa Hukumu.

iv. Kuandaa taarifa zinazohusiana na usikilizaji wa mashauri mbali mbali katika Mahkama ya Kadhi.

v. Kutoa ushauri kwa jamii kuhusiana na masuala mbali mbali yanayofikishwa katika Mahkama ya Kadhi.

**3. KADHI WA WILAYA (ZPS EX – 38)**

**NAFASI SABA (7) UNGUJA NA NAFASI TATU (3) PEMBA.**

**Sifa za muombaji**

a) Awe amehitimu shahada ya kwanza katika fani ya Sharia ya kiislamu kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.
b) Awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu katika fani ya Sharia
c) Uwezo wa kutumia Kompyuta ni sifa ya ziada itakayopewa kipaumbele.
d) Awe Mzanzibari.

**Majukumu**

i. Kusikiliza kesi za madai zinazohusiana na mambo ya kiislamu kwa mujibu wa uwezo aliopewa kisheria.
ii. Kusimamia upatikanaji wa mienendo ya kesi pamoja na utekelezaji wa Hukumu.
iii. Kuandaa taarifa zinazohusiana na usikilizaji wa mashauri mbali mbali katika Mahkama ya Kadhi.
iv. Kutoa ushauri kwa jamii kuhusiana na masuala mbali mbali yanayofikishwa katika Mahkama ya Kadhi.

**4. AFISA SHERIA - DARAJA LA II (ZPSE - 10)**

**NAFASI SITA (6) UNGUJA NA NAFASI NNE (4) PEMBA.**

**Sifa za muombaji**

a) Awe amehitimu shahada ya kwanza katika fani ya Sheria kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

b) Uwezo wa kutumia Kompyuta ni sifa ya ziada itakayopewa kipaumbele.
c) Awe Mzanzibari.

**Majukumu**

i. Kukaa na Jaji/ Hakimu wakati wa kuendesha kesi.
ii. Kutayarisha decree na drawn order pale kesi inapomalizika.
iii. Kutoa hati za wito (Summons) za kuwaita wahusika.
iv. Kutunza majalada yote ya kesi zinazoendeshwa na Jaji/Hakimu kwa kesi zinazoendelea na kumalizika.
v. Kufanya utafiti wa kesi za awali na rufaa .
vi. Kufanya utafiti wa kisheria na kutoa ushauri.
vii. Kuingia Mahkamani, kurekodi mwenendo mzima wa kesi na kuweka kumbukumbu sahihi za mashauri yanayosikilizwa na Jaji.
viii. Kuandika rasimu ya hukumu kwa kesi za awali na rufaa.

**5. MSULUHISHI DARAJA LA II (ZPSE -10)**

**NAFASI TANO (5) UNGUJA NA NAFASI SITA (6) PEMBA.**

**Sifa za muombaji**

a) Awe amehitimu shahada ya kwanza au stashahada katika fani ya ushauri nasaha, saikolojia, elimu ya jamii au fani yoyote inayofanana na hizo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali ya mapinduzi Zanzibar.
b) Awe na elimu na uzoefu katika sharia za kislamu
c) Uwezo wa kutumia Kompyuta ni sifa ya ziada itakayopewa kipaumbele.

d) Awe Mzanzibari.

**Majukumu**

i. Kupokea mgogoro kutoka mahkamani kwa ajili ya kusuluhisha.
ii. Kuwezesha mawasiliano baina ya wadaawa katika mgogoro.
iii. Kuainisha kiini cha mgogoro katika suluhu anayoisimamia, kutambua maeneo ya maelewano, pamoja na kuongoza majadiliano baina ya wadaawa kwa njia ya usawa na amani.
iv. Kuwasaidia wadaawa kufichua, au kuwaongoza katika, mbinu za kufikia suluhu inazoendana na viwango vya kisheria, mahitaji ya msingi katika mgogoro na maslahi ya pande zote.
v. Kuwezesha pande zinazohusika na kesi mbele ya mahkama kufikia suluhu inayokubalika na pande zote bila ya kuendelea na kesi mahkamani.
vi. Kuandika masharti ya makubaliano iwapo wadaawa wamefikia suluhu ya amani, na kuyawasilisha mahakamani kwa lengo la kurekodiwa kama amri au hukumu ya mahkama.
vii. Kurejesha mgogoro mahkamani kwa kuendelea na kesi ya msingi iwapo wadaawa wameshindwa kufikia suluhu.
viii. Kulinda haki na usalama wa wadaawa kwa kuhakikisha usiri katika hatua zote za usuluhishi.

**6. KATIBU MUHTASI DARAJA LA III (ZPSD-01) NAFASI SITA (6) UNGUJA NA NAFASI NNE (4) PEMBA.**

**Sifa za muombaji**

a) Awe amehitimu stashahada katika fani ya uhazili kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

b) Awe na uwezo mzuri wa kutumia kompyuta.

c) Awe Mzanzibari.

**Majukumu**

i. Kupiga chapa nyaraka za siri, madokezo, taarifa na nyaraka nyengine.
ii. Kutunza taarifa na kumbukumbu za matukio mbalimbali.
iii. Kutunza kumbukumbu za wageni, tarehe za vikao na ratiba ya kazi nyengine zilizopangwa.
iv. Kutunza majalada au nyaraka nyengine za ofisi yake.

**7. DEREVA -DARAJA LA III (ZPSB 06) NAFASI NANE (8) UNGUJA NA NAFASI MBILI (2) PEMBA.**

**Sifa za muombaji**

a) Awe amehitimu kidatu cha Nne (F.IV)

b) Awe na leseni ya udereva inayotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

c) Cheti cha Jeshi la Kujenga Uchumu (JKU) na mwenye ujuzi wa ufundi wa magari ni sifa ambazo zitapewa kipaombele.

d) Awe Mzanzibari.

**Majukumu**

i. Kukagua gari aliyopangiwa kazi kabla ya kutumika kila siku.
ii. Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote.
iii. Kujaza (Log book) kabla ya kufanya safari alliyopangiwa.

iv. Kutoa taarifa kwa mkuu wake wa kazi juu ya haja ya kufanyiwa matengenezo gari baada ya kumjulisha tatizo la gari ambayo imepata maharibiko.
v. Kuwa tayari kufanya safari yoyote ya kazi na kwa wakati atakaopangiwa na mkuu wake.
vi. Kuwa na kumbukumbu ya wakati wa gari kupelekwa garage kwa ajili ya kufanyiwa "General Service".

**JINSI YA KUOMBA**

1. Kwa waombaji ambao ni wajiriwa wa Serikali maombi yao yawasilishwe moja kwa moja katika Ofisi za Tume ya Utumishi ya Mahkama zilizopo Mahkama Kuu Unguja (Tunguu) na Mahkama Kuu Pemba (ChakeChake) muda wa saa za kazi kupitia anuwani ifuatayo:

   **KATIBU**
   **TUME YA UTUMISHI YA MAHKAMA**
   **214 BARABARA YA TUNGUU**
   **70491 KUSINI UNGUJA**
   **ZANZIBAR.**

   **a)** Barua za maombi ziandikwe kwa Mkono na ziambatanishwe na:
   i. Maelezo binafsi ya muombaji (CV)
   ii. Kivuli cha cheti cha kuzaliwa.
   iii. Kivuli cha cheti cha kumalizia masomo.
   iv. Kivuli cha kitambulisho cha Mzanzibar.
   v. Picha mbili (2) za passport size zilizopigwa karibuni.
   vi. Pamoja na barua ya ruhusa ya Mkuu wako wa Kazi isipokuwa waajiriwa wa Mahkama tu.

2. Kwa waombaji ambao hawakuajiriwa na Serikali maombi yao yawasilishwe moja kwa moja kupitia Mfumo wa ZanAjira portal.zanajira.go.tz/home. Kupitia anuwani ifuatayo:

**KATIBU**
**TUME YA UTUMISHI YA MAHKAMA**
**214 BARABARA YA TUNGUU**
**70491 KUSINI UNGUJA**
**ZANZIBAR.**

**a)** Barua za maombi ziandikwe kwa Mkono na ziambatanishwe na:

i. Maelezo binafsi ya muombaji (CV)
ii. Kivuli cha cheti cha kuzaliwa.
iii. Kivuli cha cheti cha kumalizia masomo.
iv. Kivuli cha kitambulisho cha Mzanzibar.

Tangazo hili pia linapatikana kwenye tovuti ya Mahkama www.judiciaryzanzibar.go.tz. Na Portal ya ZanAjira portal.zanajira.go.tz/home

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 21/07/2026 muda wa saa za kazi.